Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 04 Issue: 01 | October-2025

EAJK

# Usimilisho wa Tenzi za Kale kama Njia ya Kukuza Uelewa wa Utamaduni na Historia kwa Watoto: Mfano wa Tenzi Za *Fumo Liyongo* na *Mwana Kupona*

**Authors**
**Evangeline Makena Mitambo [(1)]; Dorcas M. Musyimi [(2)]; Allan Mugambi [(3)]**
**Main author's email: evamitambo@gmail.com**

**(1.2.3) Chuka University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Mitambo, E. M., Musyimi, D. M., & Mugambi, A. (2025). Usimilisho wa tenzi za kale kama njia ya kukuza uelewa wa utamaduni na historia kwa watoto: Mfano wa tenzi za *Fumo Liyongo* na *Mwana Kupona*. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 4* (1), 76-88. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.849

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2025-08-13
Accepted: 2025-09-11
Published: 2025-10-14

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2025 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Tenzi za kale za Kiswahili ni hazina ya urithi wa historia na utamaduni wa Waswahili. Tenzi hizi zilitungiwa hadhira ya watu wazima. Aghalabu zimesheheni lugha ya kale, mitindo tata ya kishairi na maudhui ya kifalsafa na kidini. Hivyo, ni ngumu kwa watoto kuelewa tenzi za kale. Hali hii ni changamoto kwa watoto kupokea utamaduni na historia ya Waswahuli. Wasanii wa kisasa wamefanya jitihada kusimilisha tenzi hizo kuwa fasihi ya watoto. Hata hivyo, tafiti hazijachunguza kwa kina usimilisho kama njia ya kuwasilisha utamaduni na historia. Makala hii imechunguza usimilisho wa tenzi za kale kama njia ya kukuza uelewa wa historia na utamaduni kwa watoto. Tenzi mbili; *Fumo Liyongo* na *Mwana Kupona* zilizingatiwa. Aidha, masimilisho ya tenzi teule; *Kisa cha Fumo Liyongo* (KcFL), *Mkasa wa Shujaa Liyongo* (MwSHL) na *Wasifu wa Mwana Kupona* (WwMK) yalitumika. Data ya utafiti ilikusanywa kupitia usomaji makini wa matini chaili na matini lengwa. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa misingi ya Nadharia ya Usimilisho ya Hutcheon (2013). Utafiti ulibaini kuwa historia ya mashujaa, mifumo ya kiutawala, dini, sherehe, vyakula na mavazi viliundwa upya kwa njia nyepesi na picha za kimaelezo ili kufaa hadhira ya watoto. Hivyo, usimilisho ulichangia katika kukuza ufahamu wa kitamaduni na kihistoria kwa vizazi vijavyo. Makala hii inapendekeza watafiti wa baadaye wachunguze kazi nyingine za usimilisho wa tenzi za kale kutoka tamaduni tofauti za Kiafrika.

**Maneno muhimu:** Fasihi ya watoto, historia, masimilisho, tenzi za kale, usimilisho, utamaduni.

**UTANGULIZI**

Fasihi ya watoto ni tawi la fasihi linalolenga hadhira ya watoto kwa ajili ya burudani, elimu, mafunzo ya maadili na uendelezaji wa utamaduni. Kimsingi, fasihi ya watoto hutumia lugha rahisi, sura fupi, wahusika wa kuvutia na mazingira yanayojulikana na mtoto ili kufikisha ujumbe kwa ufasaha (Wamitila, 2008). Fasihi hii ni taaluma inayojisimamia, ingawa mizizi yake ipo katika fasihi kwa jumla. Kulingana na Jan (1969), fasihi ya watoto imekuwa hai na inaendelea kuwa hai. Maelezo haya yanaashiria kwamba, baadhi ya vitabu huwavutia watoto na upokezi huo unatilia nguvu ukweli kwamba fasihi ya watoto ipo na inaendelea kukua. Mashirika ya uchapishaji kama Sasa Sema yamechangia pakubwa katika ukuaji huu kwa kuchapisha vitabu mahususi vya watoto.

Maelezo haya yalisaidia kuonyesha kwamba fasihi ya watoto ni chombo muhimu cha kijamii kinachochangia katika ujenzi wa utu, maadili na utambulisho wa kitamaduni wa mtoto. Aidha, yalisaidia kueleza kwamba usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto ni mwendelezo wa juhudi za kukuza na kuimarisha fasihi hii ili iwafikie watoto kwa njia rahisi na ya kuvutia. Hivyo, marejeleo haya yalitoa msingi wa kihistoria na kitaaluma unaounga mkono hoja kuu ya utafiti huu kwamba fasihi ya watoto ni nyenzo muhimu ya uwasilishaji wa historia na utamaduni kwa hadhira changa.

Licha ya mchango huu mkubwa, bado kuna changamoto kuhusu jinsi urithi wa kifasihi wa jadi, kama vile tenzi za kale unaweza kusimilishwa kuwa fasihi ya watoto bila kupoteza maana, maadili na uhalisia wa kihistoria na kitamaduni. Baadhi ya tafiti zimeangazia fasihi ya watoto kama tawi huru, lakini kuna pengo la kitaaluma kuhusu kiwango ambacho usimilisho wa tenzi za kale umeweza kuwasilisha historia na utamaduni wa Waswahili kwa watoto kwa njia inayoendana na uwezo wao wa kuelewa. Hivyo, utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto.

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Usimilisho wa Hutcheon (2013). Nadharia ya Usimilisho inaeleza kuwa, usimilisho ni mchakato wa ubunifu unaobadilisha kazi ya fasihi asilia kwa kuizingatia muktadha mpya wa kijamii, kihistoria au kiumri. Kupitia nadharia hii, mtafiti alichunguza namna watunzi wa kisasa wanavyosimulia upya tenzi za kale ili ziweze kueleweka, kuvutia na kuwafaa watoto kama hadhira mpya. Kwa msingi huo, lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto kunawezesha uwasilishaji wa utamaduni na historia.

Ingawa tenzi za kale za Kiswahili kama *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Utenzi wa Mwana Kupona* ni hazina kubwa ya historia na utamaduni wa Waswahili, asili yake haikulenga hadhira ya watoto bali watu wazima. Lugha yake ni ngumu, yenye mafumbo, tashbiha za kifalsafa na misemo ya kitamaduni ambayo watoto hawawezi kuielewa kwa urahisi. Hali hii imezua changamoto ya jinsi maarifa ya kihistoria na kitamaduni yaliyo katika tenzi hizo yanaweza kurithishwa kwa vizazi vipya. Usimilisho wa tenzi hizo kuwa fasihi ya watoto mathalani: *Mkasa wa Shujaa Liyongo*, *Kisa cha Fumo Liyongo* na *Wasifu wa Mwana Kupona* umejitokeza kama mbinu ya kufanikisha urahisishaji wa lugha, mabadiliko ya muundo na uondoaji wa dhima nzito za kifalsafa ili kuibua simulizi rahisi, za kuvutia na zinazoweza kufundisha watoto. Hata hivyo, kuna pengo la kitaaluma kuhusu kiwango ambacho usimilisho huo umeweza kuwasilisha historia na utamaduni wa Waswahili kwa watoto bila kupoteza uhalisia wa kazi asili. Utafiti uliopo umejikita zaidi katika kueleza mbinu za usimilisho bila kuchunguza kwa kina matokeo ya mabadiliko hayo katika uwasilishaji wa historia na utamaduni. Hivyo, utafiti huu ulichunguza namna ambavyo tenzi za kale zimebadilishwa kupitia usimilisho ili kulenga hadhira ya watoto bila kupoteza utambulisho wa kihistoria na kitamaduni wa Waswahili.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Baker (2001) anaeleza kuwa usimilisho ni aina ya tafsiri inayozidi tafsiri ya moja kwa moja kwa kuwa inahusisha ubunifu, uboreshaji na ukarabati wa matini asilia ili kuendana na mazingira mapya ya kijamii, kitamaduni na kihadhira ya hadhira lengwa. Usimilisho kama unavyoelezwa na Baker una uhusiano wa karibu na utafiti huu kwa kuwa wote wanahusisha mchakato wa kubadilisha matini chasili ili kuunda maana mpya katika muktadha tofauti. Uhusiano uliopo kati ya mawazo ya Baker (2001) na utafiti huu unaonekana katika msingi wa dhana ya mabadiliko ya ubunifu yanayolenga kufasiri upya fikra, mitazamo na maadili ya kazi asilia kwa mujibu wa mahitaji ya hadhira mpya.

Pamoja na uhusiano huo, kuna tofauti kati ya mtazamo wa Baker (2001) na mwelekeo wa utafiti huu. Baker (2001) alijadili usimilisho katika muktadha wa tafsiri baina ya lugha, akisisitiza jinsi tafsiri hubeba na kuwasilisha maana kutoka lugha moja hadi nyingine kwa kuzingatia muktadha wa kitamaduni wa hadhira lengwa. Kwa upande mwingine, utafiti huu ulishughulikia usimilisho ndani ya lugha moja, yaani, Kiswahili, lakini katika mazingira tofauti ya kihadhira.

Katika utafiti huu, usimilisho hauhusiani moja kwa moja na tafsiri ya lugha, bali ni mchakato wa kubadilisha kazi ya kifasihi kutoka hadhira ya watu wazima hadi hadhira ya watoto. Mabadiliko hayo yanahusu vipengele vya lugha, maudhui, wahusika, dhamira na mitazamo ya kifasihi ili kuendana na saikolojia na kiwango cha uelewa wa watoto. Mawazo ya Baker (2001) yalichangia katika kuimarisha msingi wa kinadharia wa utafiti huu. Yalimwekea mtafiti msingi wa dhana ya mabadiliko ya ubunifu kwa kueleza kuwa usimilisho ni mchakato wa kubuni upya unaolenga kufaa hadhira mpya. Lhermitte (2005) anasisitiza kuwa usimilisho na tafsiri zote ni njia za mawasiliano zinazohamisha ujumbe kutoka matini moja hadi nyingine kwa kudumisha uhalisia wa ujumbe. Mtafiti alitumia mtazamo huu kubaini jinsi tenzi za kale kama *Fumo Liyongo* na *Mwana Kupona* zilivyobadilishwa kuwa masimulizi rahisi yanayowaelekeza watoto kuelewa historia na utamaduni wao.

Aidha, Punzi (2007) katika utafiti wake kuhusu usambazaji wa fasihi kupitia vyombo vya habari anatoa mchango katika kuelewa dhana ya usimilisho kupitia mtazamo wa mwingiliano wa njia za mawasiliano. Punzi anaeleza kuwa pale ambapo ujumbe wa kifasihi huvuka mipaka inayotenganisha njia tofauti za mawasiliano kama vile kutoka katika maandishi kwenda katika picha, muziki au tamthilia, hali hiyo huitwa mwingiliano wa njia za mawasiliano. Hii ina maana kwamba, kazi ya kifasihi inaweza kufasiriwa kutoka mfumo mmoja wa mawasiliano hadi mwingine na mabadiliko hayo yakaleta sura mpya inayoweza kutambulika kama kazi tofauti lakini yenye asili ileile. Kama anavyosema Punzi (2007), uvukaji wa mipaka ya njia za mawasiliano ni hali ya kawaida katika historia ya fasihi na ni sawa na uvukaji wa mipaka ya tanzu za kifasihi. Hivyo, mabadiliko ya kazi ya kifasihi kutoka mfumo mmoja hadi mwingine, kama vile kutoka utenzi hadi riwaya ya watoto, ni tendo la usimilisho linaloonyesha mwingiliano wa njia za mawasiliano. Mchakato huu unahusisha kuibadilisha kazi ya awali ili iweze kufikika na kueleweka kwa hadhira mpya huku ikidumisha dhamira au ujumbe wa msingi wa kazi ya asilia. Mawazo ya Punzi yalikuwa na mchango katika utafiti huu kwa kuwa yalimwezesha mtafiti kufafanua namna usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto ulivyotumika kama njia mbadala ya mawasiliano inayofaa zaidi kwa watoto. Kupitia mtazamo wa Punzi (2007), mtafiti aliweza kuelewa kuwa mabadiliko hayo si upotoshaji wa kazi za awali bali ni urahisishaji wa njia za mawasiliano unaolenga kuwezesha watoto kuelewa historia na utamaduni wa jamii ya Waswahili kwa urahisi zaidi.

Kulingana na Dean (2009), usimilisho ni mwingiliano matini unaojitokeza pale ambapo kazi mpya huunda upya kazi za jadi kwa kuzitumia katika muktadha tofauti. Hivyo, usimilisho hauchukuliwi tu kama nakala ya kazi ya awali bali kama mchakato wa kiubunifu unaolenga kuzalisha kazi mpya inayoweza kutambulika kwa namna ya kipekee. Dean anaeleza kuwa tafsiri inayofanyika kupitia njia tofauti za mawasiliano, kama vile kutoka katika maandishi kwenda katika sinema, tamthilia au michezo ya jukwaani, ni usimilisho kwa kuwa inahusisha uhamishaji wa ujumbe kutoka mfumo mmoja wa sanaa kwenda mwingine. Dean (2009) anaongeza kwamba usimilisho hutambulika kupitia matumizi ya malighafi muhimu za kazi ya asili, mbinu tofauti za uwasilishaji na kanuni za kiubunifu zinazomruhusu msanii au mwandishi kutoa kazi mpya yenye sura na mvuto tofauti, lakini inayodumisha kiini cha kazi ya awali. Uhusiano kati ya utafiti wa Dean na utafiti huu uko katika msingi wa kidhana. Tafiti zote mbili zinachunguza mchakato wa uhamishaji wa ujumbe kutoka mfumo mmoja wa mawasiliano hadi mwingine kwa madhumuni ya kuibua kazi mpya. Utafiti wa Dean (2009) unahusu usimilisho wa kazi za kihistoria na kifasihi katika sinema, wakati utafiti huu ulihusu usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto. Licha ya tofauti hiyo ya nyanja, utafiti wa Dean kuhusu usimilisho wa historia na fasihi kama sinema ulichangia utafiti huu katika kuelewa mchakato wa usimilisho kama aina ya tafsiri inayovuka mipaka ya njia za mawasiliano.

Kupitia mawazo ya Dean (2009) mtafiti alielewa kuwa usimilisho hauishii katika kubadilisha maudhui pekee,

bali unahusisha pia mbinu za uwasilishaji, muundo wa matini, na lugha inayofaa kwa kiwango cha kisaikolojia cha hadhira husika. Kwa msingi huo, utafiti wa Dean ulimwongoza mtafiti kujadili namna ambavyo usimilisho wa tenzi za kale uliwezesha kuunda kazi za fasihi ya watoto ambazo zinachangia katika kuhimiza ujifunzaji wa kihistoria na kitamaduni kwa njia rahisi, yenye mvuto na inayoendana na ulimwengu wa watoto. Kugeuza *UwFL* kuwa *MwSHl* na *KcFL* ni kama kuubadilisha utenzi wa kishairi kuwa hadithi ya kiusimulizi sawa na jinsi Dean alivyoeleza kuhusu kubadilisha fasihi ya maandishi kuwa sinema, ambapo dhamira ya asili huhifadhiwa, lakini njia ya uwasilishaji hubadilishwa ili kuwafaa wasomaji wapya.

Naye Balodis (2012) katika utafiti wake kuhusu usimilisho wa ukweli na hadithi kama maigizo anaeleza kuwa usimilisho ni mojawapo ya mbinu ambazo watunzi wa kazi za fasihi hutumia ili kuunganisha na kugeuza tanzu mbalimbali za kifasihi. Kwa mujibu wa Balodis, usimilisho ni mchakato ambapo matini ya kifasihi inayopatikana katika utanzu mmoja hubadilishwa na kupewa sifa za utanzu mwingine, jambo linaloleta uhusiano wa ubunifu kati ya aina tofauti za fasihi. Hali hii inaifanya kazi mpya kuwa na sura tofauti na ile ya awali, lakini bado ikiendeleza misingi na dhamira za matini chasili. Balodis (2012) anaeleza kwamba, historia ya fasihi imejaa usimilisho.

Katika fasihi ya Kiswahili, tenzi mbalimbali zilisimilishwa kuwa masimulizi ya kuhadithiwa huku katika fasihi ya Kigiriki, wasanii wakigeuza hadithi za visasili na historia kuwa tamthilia. Vilevile, Shakespeare alitumia mbinu za usimilisho kusimulia upya hadithi za mapenzi na visa vya kihistoria kutoka kwa waandishi wengine na kuibuka na tamthilia mpya zenye mvuto mkubwa. Kwa mtazamo wa Balodis (2012), usimilisho ni njia ya ubunifu inayowawezesha wasanii kuendeleza kazi chasili kwa kuzifanyia ukarabati wa kimtindo, kimtazamo na kimaudhui ili kuleta kazi mpya yenye uhalisia wa kisanaa na mvuto kwa hadhira mpya. Uhusiano kati ya utafiti wa Balodis (2012) na utafiti huu uko katika msingi wa dhana ya usimilisho kama chombo cha ubunifu. Tafiti zote zinachunguza jinsi usimilisho unavyowezesha kazi mpya kuibuka kutokana na kazi za awali kupitia mchakato wa kukarabati mfumo wa uwasilishaji, lugha na hadhira inayolengwa. Tofauti ni kwamba utafiti wa Balodis ulilenga uwanja wa maigizo; yaani, jinsi hadithi na ukweli ulivyobadilishwa kuwa tamthilia, ilhali utafiti huu ulilenga uwanja wa fasihi andishi ya watoto, ambapo tenzi za kale za Kiswahili zilisimilishwa kuwa hadithi na riwaya zinazofaa watoto. Hata hivyo, kupitia mawazo ya Balodis (2012) mtafiti alifahamu kuwa usimilisho si tu mchakato wa kubadili sura ya kazi, bali pia ni mbinu ya kimaendeleo inayoweza kusaidia kukuza uelewa wa watoto kuhusu historia na utamaduni. Kubadilisha *UwFL* kuwa *MwSHL* au *KcFL* kunahusisha ukarabati wa kimaumbo na kimaudhui ambao unafanya hadithi hizo ziwe nyepesi, zenye taswira na matukio yanayovutia watoto, hivyo kutekeleza jukumu la kielimu na kitamaduni kwa urahisi zaidi.

Uchanganuzi wa mitazamo ya watafiti hawa wote ulimwezesha mtafiti kutathmini jinsi usimilisho ulivyotumika kubadilisha na kusasisha maarifa ya kihistoria na kitamaduni ya Waswahili ili yaeleweke na kuvutia hadhira ya watoto, hivyo kukuza uelewa wa historia na utamaduni kwa vizazi vipya. Hata hivyo, tafiti za awali hazijazingatia kwa kina namna usimilisho wa tenzi za kale ulivyotumika kukuza uelewa wa historia na utamaduni kwa watoto, hususan kwa kuzingatia mabadiliko ya maudhui, lugha na mitindo ili yalete maana katika fasihi ya watoto. Pengo hili la kimtazamo ndilo lililomchochea mtafiti kuchunguza kwa kina jinsi usimilisho wa tenzi za kale umechangia uelewa wa historia na utamaduni wa Waswahili miongoni mwa watoto kupitia kazi kama *KcFL*, *MwSHL* na *WwMK*.

**Msingi wa Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Usimilisho kwa mtazamo wa Hutcheon (2013). Nadharia hii ambayo chimbuko lake linahusishwa na kazi ya Bluestone (1957) aliyekuwa akichanganua filamu, inaeleza kuwa kila usimilisho huzalisha kazi huru inayojitawala, kwani katika mchakato wa usimilisho msanii anaweza kuongeza, kuondoa au kubadilisha vipengee vya kazi asilia ili iendane na muktadha mpya. Kulingana na Hutcheon (2013) sanaa hubuniwa kutokana na sanaa nyingine, na hadithi huzaliwa kutokana na hadithi nyingine, hivyo kila usimilisho ni ubunifu mpya unaoendeleza maana badala ya kuirudia.

Msingi huu wa nadharia uliwezesha utafiti huu kuchunguza jinsi tenzi za kale kama *UwFL (Mulokozi 1999)* na *UwMK (Mulokozi 1999)* zilivyopata uhai mpya

kupitia usimilisho wake katika *KcFL (King'ei, 2007)*, *WwMK (Wamitila, 2008)* na *MwSHL (Matundura, 2018)* ili kuendeleza uelewa wa historia na utamaduni kwa watoto. Kupitia mhimili wa nadharia hii kwamba kiini cha usimilisho ni hadithi, utafiti ulibainisha kuwa hadithi za kishujaa, kifalsafa na za kihistoria zilizomo katika tenzi za kale zilibadilishwa kwa namna nyepesi na yenye mvuto ili ziweze kueleweka kwa watoto. Usimulizi wa mashujaa kama Liyongo na mafundisho ya kimaadili ya Mwana Kupona ulirahisishwa bila kupoteza kiini cha utamaduni wa Kiswahili, hivyo kuwasaidia watoto kujifunza historia ya jamii yao kupitia hadithi zinazowavutia.

Kwa mujibu wa mhimili wa pili, unaosisitiza kuwa usimilisho ni mchakato wa kubadilisha hadithi kulingana na hadhira na muktadha mpya, utafiti huu ulionyesha jinsi vipengele vizito vya utamaduni na historia kama vile istilahi za kale, misemo ya kidini na masimulizi marefu ya kishujaa, vilivyosimilishwa ili viwe rahisi na vyenye kuendana na saikolojia ya watoto. Hivyo, utamaduni wa Waswahili ulihifadhiwa kwa njia nyepesi, ambapo watoto wanapata fursa ya kuelewa mila, desturi na historia ya mashujaa wa jamii yao kupitia lugha rahisi na mifano ya maisha ya kila siku. Kwa mujibu wa mhimili wa tatu, unaoona usimilisho kama ukarabati wa kina wa kazi fulani, utafiti ulionyesha kuwa mabadiliko katika muundo wa tanzu kutoka mashairi hadi nathari yalirahisisha uwasilishaji wa historia na utamaduni.

Hatimaye, mhimili wa nne, unaosisitiza kuwa usimilisho ni utafsiri upya na umbaji upya, ulisaidia kuonyesha kuwa waandishi wa kazi zilizochunguzwa hawakunakili tu maudhui ya kale, bali walitafsiri upya maana yake kwa kuipa sura mpya inayolingana na ulimwengu wa kisasa wa watoto. Kupitia tafsiri hii upya, tenzi za kale ziliweza kufanikisha uwasilishaji wa historia na utamaduni wa Waswahili katika namna inayowafundisha na kuwaburudisha watoto. Kwa hivyo, misingi ya Nadharia ya Usimilisho iliwezesha utafiti huu kufafanua kwa kina jinsi usimilisho wa hadithi za kale ulivyotumika kama mbinu ya kuendeleza uelewa wa utamaduni na historia kwa vizazi vipya.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia njia za kimaelezo, kimaudhui na kifasihi linganishi. Kwa kutumia njia ya kimaelezo, mtafiti alieleza kwa kina namna vipengele vya kihistoria na kitamaduni vilivyohifadhiwa au kubadilishwa katika masimilisho ya tenzi teule. Aidha, njia ya kimaudhui ilitumika kuchambua maudhui, wahusika, mandhari na mitindo ya lugha ili kufafanua ubadilishaji wa tenzi za kale teule ili kuendana na uelewa wa watoto. Vilevile, njia ya kifasihi linganishi ilitumika kulinganisha kazi chanzi na kazi lengwa ili kubaini uhusiano na tofauti katika uwasilishaji wa historia na utamaduni kwa watoto. Kwa kutumia mbinu hizi kwa pamoja, utafiti uliweza kuonyesha namna usimilisho wa tenzi za kale teule umechangia kuendeleza utamaduni na historia ya Waswahili kwa hadhira ya watoto.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Uelewa wa Utamaduni na Historia kwa Watoto Kupitia Usimilisho

Usimilisho wa utamaduni ni mojawapo ya mikakati muhimu katika mchakato wa kusawiri kazi za kifasihi za awali ili ziwafae watoto. Kwa mujibu wa Nadharia ya Usimilisho ya Hutcheon (2013), usimilisho huhusisha mchakato wa uumbaji upya unaotokana na kazi ya awali ambapo maana maudhui na dhamira hudumishwa au kubadilishwa ili zilingane na hadhira mpya. Katika kazi teule, usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto umehusisha uwasilishaji wa vipengele vya kiutamaduni na historia kwa njia nyepesi na ya kuvutia ili kulenga hadhira ya watoto kama ilivyojadiliwa katika vijisehemu vifuatavyo.

#### Hali ya Maisha na Mahusiano ya kijamii.

Utamaduni kama jumla ya shughuli, kumbukumbu, matumaini na mipango ya baadaye ya jamii fulani zikiwemo ndoto na maono ya jamii hiyo. Kwa mujibu wa Nadharia ya Usimilisho, usimilisho ni mchakato wa uumbaji upya ambapo msimilishi hubadilisha, huongeza au huondoa vipengele vya matini chasili ili kutoa maana mpya kulingana na hadhira lengwa. Waandishi wa masimilisho teule wamebua upya vipengele vya kijamii kama vijakazi, ndoa, uchumba, ubikira na mafunzo ya unyagoni kwa lugha rahisi inayowafaa watoto.

Katika *MwSHL (*Matundura, 2018*)* na *WwMK*, (King'ei 2008) kipengele cha vijakazi kimeongezwa kuonyesha mgawanyo wa kitabaka na uhusiano wa kifamilia, ambapo wahusika kama Sada na Kijakazi walitumika

kufafanua maisha ya kijamii ya jadi. Vipengele hivi havipo katika tenzi asilia lakini vinaonyesha jinsi jamii za kale zilivyokuwa na mfumo wa ajira za nyumbani. Vivyo hivyo, masimulizi ya ndoa na uchumba yamepanuliwa katika *WwMK (King'ei* 2008*)* na *MwSHL* (Matundura, 2018) ili kueleza mila za Waswahili kuhusu posa, mahari na mamlaka ya wazazi katika kuwaoza binti zao, jambo ambalo halikuelezwa wazi katika tenzi za kale. Mwandishi wa *WwMK* (*King'ei 2008:12)* ameongeza pia kipengele cha ubikira na utengano wa wachumba kabla ya ndoa kama ishara ya maadili na heshima, huku mafunzo ya unyagoni yakionyesha maandalizi ya wasichana kwa maisha ya ndoa na wajibu wa kifamilia. Mabadiliko haya yanadhihirisha hoja ya Hutcheon (2013) kwamba usimilisho si nakala ya kazi asilia bali ni uwasilishaji upya unaozingatia muktadha na hadhira mpya.

Kwa jumla, usimilisho wa tenzi teule uliwezesha kuwasilisha historia na utamaduni wa Waswahili kwa njia nyepesi inayowafaa watoto, ukionyesha vipengele vya kijamii, kifamilia, kitamaduni na kimaadili kwa lugha na mifumo rahisi. Hivyo, masimilisho teule yamefanikiwa kuendeleza urithi wa kitamaduni wa Waswahili huku yakifundisha watoto kuhusu maisha, mahusiano na maadili ya jamii yao kwa kutumia fasihi ya kisasa.

**Itikadi na Imani ya Dini**

Kulingana na Momanyi (2007), iikadi ni taasisi iliyo hai katika utamaduni wa jamii zote za wanadamu. Ushirikina ni sehemu ndogo katika itikadi za watu. Uganga wa hirizi na mila za kuwapa watu majina yenye maana ni Uafrika unajidhihirisha wenyewe katika matini lengwa. Kulingana na Hutcheon (2013), usimilisho si kitendo cha kunakili matini chasili pekee, bali ni kitendo cha kuunda upya maana ili kuendana na hadhira mpya. Simulizi za kale zinazohusisha hirizi, majini na itikadi nyingine zimebadilishwa na kuwasilishwa katika fasihi ya watoto kwa lugha rahisi, vielelezo vya moja kwa moja na mifano ya kila siku ambayo watoto wanaweza kuifuatilia. Katika *WWMK* (*King'ei 2008:* 10), dhana nzito za kishirikina na hirizi zimesawiriwa kupitia mazungumzo ya moja kwa moja kati ya mwalimu na wanafunzi wa marika. Badala ya maelezo marefu ya kifalsafa yaliyokuwa katika utenzi chasili, watoto wanaelezwa kwa mfano wa vijaluba vyenye maji machafu ili kufahamu dhana ya hirizi. Hii ni mbinu ya usimulizi rahisi inayolingana na uwezo wa kisaikolojia wa watoto.

> *Mwalimu alitueleza kuhusu hirizi. Msichana mmoja alituchekesha sana alipomwuliza mwalimu kwa nini tuwe tunabeba hirizi chafu kama vile vijaluba vyenye maji machafu viunoni au migongoni mwetu kila mahali tuendapo... Hirizi ni aina ya vifaa vinavyovaliwa mwilini ndani ya nguo, mikononi au shingoni kwa imani kuwa vinaweza kumlinda mvaaji dhidi ya jicho la hasidi au mchawi.*
> (King'ei, 2008, uk. 10)

Kulingana na Hutcheon, kila usimilisho una ajenda mpya ya kimaana. Katika masimilisho teule, iamani za jadi hazikukusudiwa tu kuwa hadithi za kale bali ni nyenzo za malezi ya kiutamaduni. Mfano, kauli ya Mwana Kupona kwamba "hirizi hutulinda kutokana na maovu ya shetani" si maelezo ya kishirikina pekee bali ni njia ya kufundisha watoto kwamba, jamii zao zilikuwa na imani ya ulinzi na maadili ya kiroho. Jamii ya Lamu walitengeneza hirizi kwa kaure au punje za shanga. Mwalimu wa marika alieleza kuhusu hirizi ya kipochi au kifuko kidogo cha ngozi chenye maji yaliyochanganywa na vipande vya maandishi ya Korani. Vilivaliwa kwa uzi kiunoni ndani ya nguo. Waliovaa waliamini kuwa hirizi ile iliweza kumsitiri kila aliyevaa kutokana na maradhi au mikosi yoyote. *"Hirizi hutulinda kutokana na maovu ya shetani"* (King'ei, 2008, uk. 12).

Katika *KCFL*, kuzaliwa kwa Liyongo kwa namna ya ajabu (akinywa debe zima la maziwa) kumeendelea kuhifadhi dhana ya imani za kijini. Simulizi za majini ni ithibati ya sanaa jadi ya Waswahili. Hata hivyo, simulizi hili limewasilishwa kwa mtindo wa kitendawili na mshangao, jambo linalofanya watoto wajifunze kuhusu dhana ya majini kwa njia ya hadithi ya kuvutia. Huu ni usimilisho wa imani ya kijadi kuwa simulizi ya kusisimua kwa watoto.

> *Wakauzana kuna nini, huyu mwana ama jini;*
> *Haya maziwa jamani, yote katia tumboni;*
> *Hili tumbo lina nini, shimo au kitu gani?*
> *Hadithi ya Fumo Liyongo...*
> (Wamitila, 2007, uk. 1)

Dondoo hili linanyesha kwamba, imani katika itikadi na utamaduni wa jini umeifadhiwa wa kuendelezwa na watu wengi katika jamii za Kiafrika. Hii inawafundisha watoto kuhusu imani za jadi na dhana za viumbe visivyo vya kawaida au wenye nguvu za ajabu vilivyokuwa katika jamii za zamani, ikijumuisha sehemu muhimu ya urithi wa kitamaduni.

Njogu na Chimerah (1999) wanasisitiza kuwa mwandishi ni zao la jamii na hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake. Kwa hivyo, katika usimilisho, waandishi wamechukua imani za dini na itikadi za jadi zilizokuwa kwenye tenzi na kuziweka kwenye riwaya za watoto ili watoto wajenge utambulisho wa kitamaduni. Hii inalingana na hoja ya Hutcheon kwamba usimilisho ni kitendo cha kuhuisha urithi wa kifasihi kwa mazingira mapya. Kwa kuzingatia Nadharia ya Usimilisho inabainika kwamba, imani za dini na itikadi kama hirizi na majini zimechukuliwa kutoka kwenye tenzi chasili na kusawiriwa kwa namna rahisi, yenye ucheshi, simulizi na picha rahisi kueleweka. Hii inamwezesha mtoto kuzielewa si kwa uzito wa kifalsafa bali kama sehemu ya urithi wa jamii zao na somo la maadili.

**Utamaduni wa Kibaharia na Kipwani**

Kwa mujibu wa Mbaabu (1985), utamaduni ni mkusanyiko wa mila, jadi, desturi, imani, mavazi na maisha ya jamii. Huu ndio msingi wa fasihi. Utamaduni wa Waswahili umejengeka sana katika mazingira ya mwambao. Bluestone (1957) anabainisha kuwa, usimilisho ni kitendo cha kubadilisha kazi fulani kwa kuzingatia muktadha mpya, hadhira mpya na kusudi jipya. Hii ndiyo dhana inayoonekana wazi katika masimulizi ya *KcFL*, *MwSL* na *WwMK*, ambapo vipengele vya maisha ya Kibaharia na Kipwani vimebadilishwa na kurahisishwa ili kumfaa msomaji mtoto. Tenzi za kale zimebadilishwa ili kutumiwa kama njia ya kukuza uelewa wa kihistoria na kitamaduni kwa watoto. Katika *KcFL* Liyongo anaonyeshwa akikabiliana na mamba majini. Kwa asili, hili ni tukio la kishujaa lenye uzito wa kifalsafa kuhusu vita kati ya mwanadamu na asili. Katika *MwSHL*, simulizi hilo linawasilishwa kwa lugha nyepesi na ya moja kwa moja.

> *Siku moja Liyongo na marafikize walikuwa katika ufuo wa bahari wakicheza. Ndipo ghafla kama mauti, akatokea mamba mmoja mkubwa na kuunasa mguu wa kijana huyo.*
> (Matundura, 2018, uk. 14)

> *Liyongo kashufu mtoni, atambue kunanini;*
> *Ni mwanamke majini, mamba mem'uma kinywani;*
> *Tena ni mamba kaini, nyama kubwa la uzani;*
> *Hadithi ya Fumo Liyongo...*
> (Wamitila, 2007, uk. 3)

Kwa mujibu wa Hutcheon, mabadiliko haya ni mfano wa kubadilisha hadithi ili kuendana na saikolojia ya hadhira mpya. Tukio ambalo lingekuwa giza na la hofu katika utenzi wa kale, limepunguzwa ukali wake ili mtoto aweze kujifunza kuhusu hatari za bahari na heshima kwa viumbe bila kuogopa sana. Wahusika kama vile Liyongo katika *MwSL* na *KcFL* ni umbuji wa utamaduni ambao ni kielelezo cha wenyejiwa kiasili wa jamii ya Waswahili wa Mwambao wa Kaskazini, Kenya. Wanajamii walitegemea upepo ili kuweza kusafiria baharini. Katika *WwMK*. Kitwana na Mwana Kupona wanazungumzia maandalizi ya safari ya baharini. Inabidi wahakikishe maji yamejaa na kuzingatia upepo. Mwana Kupona katika *WwMK* anamwagiza kitwana amweleze baharia Salim atayarishe mashua muda atakapojua maji yatajaa.

> *Salim alisema kuwa maji yatajaa mapema, mara tu baada ya jua kuchomoza." "Vyema. Naomba umweleze Salim atayarishe mashua kwa safari wakati huo.*
> (King'ei, 2008, uk. 63)

> *Usisahau kuzingatia upepo ili tusije pata tu siyoyalalia wala kuyaamkia.*
> (King'ei, 2008, uk. 77)

Haya ni maneno ya Kitwana na Mwana Kupona mtawalia. Kupitia maelezo haya, mtoto anafahamu kuwa usafiri hutegeme hali ya bahari. Waswahili walitumia mashua kusafiria kama mojawapo ya utamaduni wao. Mtoto anaposoma riwaya ya *WwMK*,anaweza kuelewa utamaduni wa Waafrika hasa wa Mwambao ambao unahusu maisha yao ya usafiri. Kupitia usimilisho mtoto anafunzwa kuwa, usafiri wa Waswahili ulitegemea upepo na mawimbi, jambo ambalo ni msingi wa utamaduni wa Kibaharia. Kwa kutumia dhana ya Hutcheon (2013) ya kubadilisha na kuhamisha maana tunaelewa kuwa, simulizi la safari

siyo tu kielelezo cha kiutamaduni bali pia limepangwa kama fundisho la moja kwa moja kwa mtoto kuhusu kupanga, subira na kujifunza kuhusu mazingira ya asili.

Mijengo, mimea ya pwani na bahari vinavyoonekana kwenye jalada la *WwMK* na *KcFL* ni sehemu ya mbinu za usimilisho wa kisanaa. Hutcheon anasisitiza kuwa usimilisho si tu maandishi bali pia ni vielelezo na maonyesho vinavyowekwa ili kuvutia hadhira mpya. Hapa, michoro na mandhari ya kifasihi inafanya kazi ya kukuza uelewa wa mtoto kuhusu mazingira ya pwani. Katika utenzi wa kale, Fumo Liyongo anatajwa akiangusha makoma kwa uta na mshale. Kitendo hiki, katika usomaji wa watoto, kinapata maana mpya kuwa ni ishara ya uhusiano wa Waswahili na mimea ya pwani. Kwa mujibu wa Hutcheon, hii ni kubadilisha ishara na alama ili ziwe rahisi kueleweka kwa mtoto. Kwa mujibu wa TUKI (2013), utamaduni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. Hii ina maana kuwa, jamii yoyote ile ulimwenguni ina mambo fulani inayoweza kujitambulisha kwayo, si wakati huu tu bali tangu jadi. Mila na desturi hujengwa, hukomaa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Iwapo jambo hili halitatekelezwa, pana hatari ya kufifia kwa utamaduni au hata kutokomea kabisa. Kwa kusimilisha tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto, waandishi wa masimilisho teule wamefanikiwa kuwasilisha utamaduni wa waswahili kwa hadhira ya watoto. Kwa kusimilisha tenzi za kale, waandishi wamegeuza simulizi tata za bahari, mashujaa na maisha ya pwani kuwa hadithi zinazomfunza mtoto kuhusu utamaduni wa Kibaharia wa Waswahili.

**Mapokezi ya Hadithi (Simulizi)**

Hadithi ni njia ya msingi ya kusimulia maarifa, utamaduni na historia ya jamii. Kulingana n Nadharia ya Usimilisho (Hutcheon, 2013), hadithi ndicho kiungo muhimu cha usimilisho. Kila usimilisho huibua sehemu ya utamaduni unaohusishwa na usimilisho huo. Uwakilishaji wa kitamaduni ni sehemu muhimu ya usimilisho na kile kinachofanyika katika vipengele muhimu vinavyounda hadithi. Ingawa masimilisho hubadilika kwa kila usimuliaji ili kulingana na misingi ya utamaduni wa jamii ya sasa, kuna baadhi ya vipengele vya hadithi ambavyo lazima vidumishwe ili kuibua athari ile ile ya matini chasili. Katika fasihi ya watoto, hadithi zinatumika kama njia ya kufundishia na kuelimisha watoto kuhusu mambo mbalimbali katika jamii. Kwa kuwasimulia hadithi za kale zilizosimilishwa kuwa fasihi ya watoto, watoto wanapata fursa ya kujifunza kuhusu historia na utamaduni wa jamii yao. Nadharia ya Usimilisho inashikilia kuwa, majadiliano ya hadithi hupotea katika usimilisho bali visawe vya hadithi kama vile ishara, maudhui, matukio, wahusika na uhusika, mitazamo na muktadha hutafutwa katika mifumo tofauti ya ishara. Katika *KcFL*, hadithi inaanza kwa kuwaalika vijana ili wasikilize.

> *Vijana karibieni, masikio yategeni; Kisa nisimulieni, yalotendeka zamani...*
> (Wamitila, 2007, uk. 1)

Hii inakisi utamaduni wa kusimulia hadithi kwa njia ya mdomo. Kupitia mishororo iliyo hapo juu, watoto wanajifunza juu ya umuhimu wa kusimulia hadithi kama njia ya kuhifadhi na kupitisha maarifa ya kitamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Waandishi wa *KcFL*, *MwSHL* na *WwMK* wametumia nafasi ya tatu ili kusimulia hadithi yao. Wamefaulu katika kumweleza mtoto mambo mengi kuhusu tabia na mienendo ya wahusika waliotumika katika masimilisho teule. Aidha, wameweza kumweleza mtoto kuhusu mandhari tofauti tofauti ambamo matukio ya hadithi yamejikita. Katika *Kisa cha Fumo Liyongo* na *Mkasa wa Shujaa Liyongo,* waandishi wameeleza mandhari ya pwani alikoishi babake Liyongo, Fumo. Hadithi katika masimilisho teule yanamtaja Liyongo kuwa alizaliwa pwani na kuishi huko sehemu za pwani.

> *Alikuwa bado akiyatafari maisha yake kama Mfalme wa Shanga alipogutushwa na sauti ya mwanawe, Liyongo akimwita.*
> (Matundura, 2018, uk. 2)

> *Ilivyokuwa desturi ya wakati huo, mtu yeyote aliyeoa kutoka kabila tofauti alikubaliwa kwenda kuishi na watu wa kabila la mke wake. Shinda alimshawishi Liyongo waende wakaishi miongoni mwa watu wa ukoo wake – Wagalla. Mbeleni Liyongo alipinga haya vikali. Shida alianza kulialia na na kudai kuwa Liyongo hakumpenda. Huku akiwa amelemewa na mapenzi, Liyongo alilazimika kukubali hatimaye. Mipango ya safari ya kwenda Pate ilianza. Pate ni mji ambako jamaa ya Shida iliishi.* (Matundura, 2018, uk. 26)

Dondoo lililo hapo juu linawapa watoto picha ya maisha ya jamii za pwani ya Kenya ya zamani, zikiwemo tofauti za kijamii na kiuchumi. Aidha, katika *Wasifu wa Mwana Kupona*, mwandishi ameeleza sehemu na miji ya Pate alikopita Mwana Kupona katika safari yake ya kwenda Lamu kumtembelea Fatuma rafikiye. Katika riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo*, wandishi anataja jamii mbalimbali za Kiafrika. Anaonyesha shughuli na mambo mbalimbali yaliyofanywa na jamii za Pate. Anaonyesha masuala yanayohusiana na sherehe ambazo zilijumuisha nyimbo na ngoma ambazo zilikuwa zikifanywa na wanajamii wa Pate.

> *MwanaKupona alifurahi kuwa anafanya ziara ya Pate wakati huu. Alifahamu moyoni mwake kuwa siku zake za kuishi hapa duniani zilikuwa zinakaribia kikomo. Kwa hivyo, alihitaji kumzuru mwandani wake wa tangu ujanani, Fatuma aliyeishi kisiwani Pate.*
> (King'ei, 2008, uk. 65)
>
> *Nahodha alipiga makasia akisaidiana na wenzake wawili na kuiongoza mshua hadi kwenye kivuko. Hii ndiyo iliyokuwa njia ya vyombo au mlango, kama wenyeji walivyouita ujia mpana katikati ya visiwa vya Lamu na Manda.*
> (King'ei, 2008, uk. 67)
>
> *Walipofika mwishoni mwa kisiwa cha Manda, kwa mbali waliweza kuwaona wavuvi wachache wakisimama juu ya maji kwenye misitu ya mikoko kando ya pwani.*
> (*King'ei, 2008,* uk. 68)
>
> *Mashua ilipofika mwisho wa kisiwa cha Manda kwa upande wa kushoto, nahodha Salim, aliigeuza na kuielekeza kaskazini mashariki ili kukabili kisiwa cha Pate. (King'ei, 2008,* uk. 71) *Safari ya kutoka pwani Manda hadi Pate kisiwani ilikuwa ya kuchosha na ulikuwa mwendo wa saa nne.*
> (King'ei, 2008, uk. 72)

Kupitia masimulizi haya, watoto wanajifunza kuhusu utamaduni wa jamii za kipindi hicho.

**Mandhari na Vyakula**

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa, mandhari hueleza ni wapi kazi ya fasihi ilitumika kijiografia, wakati wa kihistoria na ilihusu kina nani. Naye Wamitila (2002) anashadidia malelezo ya Njogu na Chimerah anaposema, mandhari bi ile hali ambayo hutufichulia ni wapi na ni lini matukio ya fasihi yalifanyika. Mandhari hufichua wakati na sehemu matukio yalipotokea. Mandhari yanayosawiriwa katika jalada la mbele la kitabu cha *WwMK* yanawasilisha utamaduni wa Waswahili hasa kutokana na mimea, bahari, mavazi na lugha ya Kiswahili hasa iliyotumika na mtunzi katika utenzi ulio kwenye jalad la riwaya ya *WwMK.* Fasihi ya kiswahili inatoa istiari zake kutokana na miti. Hadithi inataja majina halisi ya maeneo muhimu ya kihistoria na kitamaduni kama vile Pate na pwani kama inavyodhihirika katika dondoo lifuatalo. Mwandishi anasisitiza kuwa ni Kenya kaskazini.

> *Vijana karibieni, masikio yategeni;*
> *Kisa nisimulieni, yalotendeka zamani;*
> *Huko sehemu za pwani, ni Kenya kaskazini;*
> *Hadithi ya Fumo Liyongo..."*
>
> *Liyongo nakwambieni, alizaliwa zamani;*
> *Hakuna alo yakini, kwamba kazaliwa lini;*
> *Lakini ni huko pwani, ndiyo yake maskani;*
> *Hadithiya fumo Liyongo...*
> (Wamitila, 2007, uk. 1)
>
> *Ikenda mpaka pwani, kwa mfalume nchini;*
> *Naye hapo katamani, Liyongo aje machoni;*
> *Ajue huyo ni nani, asifiwaye vinywani'*
> *Hadithi ya Fumo Liyongo...*
> (Wamitila, 2007, uk. 7)

Mishororo iliyokolezwa rangi katika kielelezo 24a na 24b inataja majina ya miji ya kitamaduni ya Afrika. Matumizi ya majina haya yanawasaidia watoto kuweka hadithi katika muktadha halisi wa kijiografia na kihistoria, hivyo kuunganisha hadithi na eneo lao halisi na utamaduni wa Pwani ya Kenya.

Mandhari ya bahari na minazi katika *WwMK* inasisitiza uhusiano wa Mwana Kupona na maisha ya pwani ya Waswahili, ikitoa utangulizi wa mazingira aliyoyaishi na ambayo yaliathiri mawazo na ushauri wake kama inavyobainika katika sura ya tano ya *WwMK*; Safari ya Pate (*WwMK* uk 65). Mandhari ya simulizi yamejengwa

katika maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki yakiwakilisha mazingira ya jadi ya jamii ya Waswahili. Hali hii inaweza kuwasaidia watoto kutambua mazingira yao ya kitamaduni na kuyaelewa kama sehemu ya urithi wao. Kutajwa kwa Kenya kaskazini, pwani, Kipini na Galana mtoni katika *Kisa cha Fumo Liyong* kunawapa watoto ufahamu wa kijiografia wa maeneo ambapo hadithi hii zimetokea.

Katika *KcFL*, *WwMK* na *MwSHL*, usimulizi umeambatana na maelezo ya vyakula vya asili kama makoma, wali wa nazi, samaki na mihogo. Katika simulizi ya *KcFL*, wakati Liyongo anarudi mjini, watu wanazungumza kuhusu kuwa na chakula sokoni.

> *Aambiweni mjini, kuna chakula sokoni;*
> *Na halafu mwalikeni, kwenye ngoma za mjini;*
> *Ademke viungoni, na kufurahi moyoni;*
> *Hadithi ya Fumo Liyongo...*
> (Wamitila, 2007, uk. 15)

Hii inaashiria kuwa, chakula kilikuwa kinapatikana sokoni, na kinaweza kuwa kilihusishwa na sherehe na furaha za kijamii.

**Majukumu ya Kijamii na Hekima**

Katika *WwMK*, utamaduni wa kijinsia unaoelekezwa kwa wasichana umefanyiwa mabadiliko makusudi ili kuendana na hadhira ya watoto. Badala ya kuwasilisha ujumbe wa unyenyekevu unaotawala katika utenzi wa asili, toleo la watoto linaelekeza msisitizo kwenye nidhamu, heshima na kujitambua kama vipengele vya maadili ya kiutamaduni. Hili linaonyesha jinsi utamaduni wa zamani umechujwa na kuwasilishwa upya kwa njia inayowiana na maendeleo ya kijamii na saikolojia ya watoto.

Vitabu vya *KcFL*, *MwSHL* na *WwMK* ni masimulizi ya kitendi yaliyowekwa katika umbo la riwaya na mashairi mepesi ambapo wandishi wamechota visa na matukio kutoka katika *UwFL* na *UwMK* na kuweka ubunifu wake. Kulingana na nadharia ya Usimilisho, usimilisho ni tafsiri upya na umbaji upya wa kazi za fasihi. Usimilisho hufanya uzushi wa kuonyesha kuwa muundo unaweza ukatengwa na maudhui. Ubadilishaji msimbo huu unaweza kuhusisha mabadiliko ya umbo au tanzu na hivyo muktadha. Kwa kuchukua tenzi za kale na kuzibadilisha ili ziweze kufaa kwa hadhira ya watoto, kunabadilisha maana na ujumbe wa kazi hizo. Hata hivyo, maudhui ya asili ya kazi hizo hubaki yalivyo. Usimilisho hubadilisha hadithi katika mchakato wa kusimilisha ili hadithi iwafae hadhira lengwa. Kwa kubadilisha hadithi na kuzifanya ziwe rahisi kueleweka na kuvutia kwa watoto, usimilisho unawawezesha watoto kujifunza kuhusu mambo mbalimbali kwa njia inayowafaa. Mwandsihi wa *MWSL* ametumia mhusika mkuu Liyongo kama shujaa wa kitendi. Masimulizi haya ni kiwakilishi cha jamii ya Waswahili kwani mandhari, utamaduni na maisha ya Waswahili yamesawiriwa katika masimulizi haya. Mwandishi amefanikiwa kumweleza mtoto kuwa, hata Waafrika ni mashujaa na ni werevu kupitia tabia na matendo ya mhusika Liyongo, mhusika mkuu Liyongo amechorwa kama shujaa wa kitendi na mhusika wa kitamaduni kwani anasawiri masuala nyeti yanayohusu utamaduni wa jadi wa Waswahili.

**Mfumo wa Kiutawala**

Mojawapo ya dhima kuu ya usimilisho wa kazi za kale kuwa fasihi ya watoto ni kuwasilisha historia ya jamii kwa njia nyepesi, ya kuvutia na ya kufundisha. Kwa mujibu wa Starrs (2006), usimilisho huchota kutoka kwenye vyanzo vya kihistoria lakini huvibadilisha ili vilingane na mahitaji ya hadhira mpya. Kwa hivyo, historia huwa haionekani tu kama muktadha bali kama kiini cha ujenzi wa simulizi mpya kwa watoto. Kihistoria usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto kunawawezesha watoto kujua fumo wa kiutawala wa kipindi cha zamani na hali ilivyokuwa katika uongozi. Kulingana na riwaya ya *Mkasa wa Shujaa Liyongo* na mashairi ya *Kisa cha Fumo Liyongo,* mfumo wa kiutawala ulikuwa wa kifalme ambapo kuna mfalme au sultani mwenye mamlaka makubwa. Utawala huu ni wa kurithi na hufuata ukoo kama.

> *Nimwambie nini baba? Mringwari aliuliza... ufikapo huko, mfariji na kumwonyesha kwamba unamjali, asije akakufutilia mbali katika wazo la kurithi ufalme.*
> (King'ei , 2008, uk. 7)

Hili nidhihirisho kuwa ufalme uliridhishwa kulingana na ukoo. Katika *Kisa cha Fumo Liyongo*, usimulizi unaweka bayana mazingira ya kijamii ya wakati wa Liyongo: maisha ya kijiji, mifumo ya utawala, familia na ibada. Hili linawezesha watoto kufahamu historia ya jamii zao – namna maisha yalivyokuwa kabla ya ukoloni, nafasi ya wazee katika jamii, pamoja na mbinu za jadi za

kujikimu. Matukio ya kihistoria kama mapigano ya koo, njia za jadi za utatuzi wa migogoro, na nafasi ya mashairi na ngoma katika maisha ya jamii yamewekewa maelezo rahisi na ya kufundisha. Katika sura ya tatu ya *MwSHL*, tunapatana na kinyang'anyiro cha uongozi. Mhusika Liyongo anatafuta mbinu za kumng'oa Mfalme Mringwari mamalakani huku Mfalme Mringwari akitafuta njia za kumwangaiza Liyongo. Mfalme Mringwari aliyumia hila ya kumtafutia Liyongo msichana kutoka katika jamii ya Wagalla ambapo alinuia kuwatumia Wagalla kumuua Liyongo. Mringwari anatumia hila ya kumtafutia Liyongo msichana kutoka katika jamii ya Wagalla ambapo alinuia kuwatumia Wagalla kumuua Liyongo.

> *Mfalme Mringwari alipowasilisha ombi lake kwa mfalme wa Wagalla lilikubaliwa. Wanawake walipewa kazi ya kumtafuta msichana mrembo ambaye angekubalika na Liyongo na ambaye angekubali kutekeleza njama ya Mringwari.*
> (Matundura, 2018, uk. 25)

Naye Liyongo kwa upande mwingine anaunda chama pinzani cha *Operation Mringwari Out* (*OMO*) kama mbinu ya kumng'oa Mringwari mamlakani. Mwandishi amefanikiwa kuisimilisha matini chasili ya karne nyingi zilizopita na kuipa sura na mwamko mpya wa kisanaa unayoifanya matini lengwa kukifaa kipindi hiki cha kihistoria. Mwandishi ameshirikisha matukio ya kisasa kama mbinu za kuunda chama cha upinzani cha kisasa cha *operation Mringwari Out (OMO)*.

> *Miaka mitatu baada ya Mringwari kutawazwa kuwa mfalme, mambo yalianza kwenda kinyume cha matarajio. Kule kuchaguliwa kwake na baraza la wazee aushikilie ufalmewa Shanga hakukuwa kumemfurahisha Liyongo. Katika maoni yake, yeye ndiye aliyekuwa kipenzi cha babake Fumo. alitia bidii za mchwa ili aweze kuutwaa uongozi kutoka kwa Mringwari. Alitumia mbinu kocho kocho za kisiasa kumng'oa mamlakani Mringwari. Mojawapo ya mbinu alizotumia ni kuunda chama cha upinzani alichikiita Operation Mingwari Out, ama OMO kwa kifupi.* (Matundura, 2018, uk. 17)

**Miji ya Kihistoria**

Utafiti huu umebaini kuwa, masimilisho teule yamejikita katika kueleza matukio mbalimbali ya kihistoria katika jamii ya watu wa Pate. Mwandishi anataja miji ya kihistoria kama vile Pate pamoja na uwepo wa dola za kifalme ambazo zilibeba utamaduni wa utawala wa Waafrika. Vitabu cha *MwSHL* na *KcFL* vinaeleza kuhusu mfalme aliyejulikana kama Daudi Mringwari ambaye alikuwa na uchu wa madaraka na hakutaka nafasi yake ichukuliwena mtu mwingine. Ni katika misingi hii ya uongozi Mringwari alianza kumchukia Liyongo kwa kuwa alimzidi sifa.

> *Mringwari alipogundua kwamba Liyongo alikuwa na nia mbaya alikasirika sana. Mwanzoni alifikiria kuatumia majeshi yake kumtafuta na kumuua.*
> (Matundura, 2018, uk. 17)
>
> *Tangu siku hiyo, mfalme hakufikilia jingine isipokuwa jinsi ya kumkomesha Liyongo.*
> Matundura (2018, uk. 23)

Riwaya ya *MwSHL* na mashairi ya *KcFL* ni vitabu ambavyo vinasawri mivutano wa kijamii iliyokuwa barani Afrika ambapo watu waligombana wenyewe kwa wenyewe. Usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto unasaidia watoto kujua mfumo wa kiutawala wa kipindi cha zamani na hali ilivyokuwa katika ungozi.

**Kipindi cha kale**

Kupitia usimilisho, watoto wanaweza kujua masuala mbalimbali yaliyokuwa yakitokea katika jamii za kipindi cha kale. Tenzi za kale zilizosimilishwa kuwa fasihi ya watoto zinaweza kuwa zimebadilishwa ili ziweze kufaa kwa hadhira ya watoto kwani maeneo na wahusika wanaweza kubadilishwa ili kuendana na mahitaji ya hadhira ya watoto. kulingana na Nadharia ya Usimilisho, usimilisho ni mchakato wa ubunifu ambao unahitaji ujuzi na ustadi wa ubadilishaji wa kina wa kazi fulani ili ziweze kufaa kwa hadhira lengwa. Kutumia picha na michoro katika vitabu vya watoto ili kueleza matukio ya kihistoria husaidia watoto kuelewa na kukumbuka vizuri.

Katika *WwMK*, mwandishi ametumia ramani inayoonyesha baadi ya sehemu mbalimbali za Pwani kama vile Kisiwa cha Lamu, miji ya Lamu, Kisiwa cha

Manda, Kisiwa cha Manda, Kisiwa cha Pate, Mji wa Pate, Mji wa Siu, Kisiwa cha Siu na Gahari Hindi. Hizi ni sehemu ambazo Mwana Kupona alipitia katika safari take kutoka mji wa Lamu kwenda mji wa Pate ili kumjulia hali rafiki yake Fatuma na kumwachia jukumu la kumtunzia wanawe. Sehemu zilizoorodheshwa zipo katika maeneo ya Pwani, hivyo, mtoto anaelewa historia ya miji ya Pwani. Kupitia ramani iliyotumika, mtoto anaweza kupata taswira ya miji ya eneo la Pwani.

**Mashujaa wa Kiafrika**

Utenzi wa *Fumo Liyongo* umetumia mhusika shujaa wa mapisi ya Uswahilini amaye aliwai kuishi katika upwa wa Afrika Mashariki. Wazo la Liyongo kuwa shujaa wa mapisi aliyeishi katika upwa wa Afrika Mashariki linashikiliwa na Mulokozi (1999) anayeeleza kuwa.Fumo Liyongo ni shujaa wa kihistoria aliyewahi kuishi katoka maeneo ya Siu. Aidha, Mulokozi anaendelea kusema kuwa, Liyongo aliishi Pwani ya kaskazini ya Kenya kwenye maeneo ya Pate na Ozi. Mtafiti aligundua kuwa, *UwFL* umehifadhi mapisi ambayo yamesimilishwa katika riwaya ya watoto ya *MwSHL* na mashairi ya watoto ya *KcFL* mapisi ya mhusika Liyongo na maisha yake kwa jumla yameelezwa kwa kifupi katika *UwFL.* Kulingana na *UwFL*, Fumo Liyongo alizaliwa Siu, Pate na alifariki sehemu ya Mwana. Wazo hili linakubalika kuwa hiyo ni historia ya kweli inayomhusu Fumo Liyongo.

> *Ya Liyongo hukwambiya,*
> *Siu alikozaliwa,*
> *Pate akitembeleya,*
> *Kwa Mwana akafiliya.*
> (Mulokozi, 1999, uk. 230)

Usimilisho hubadilisha hadithi katika mchakato wa kusimilisha ili hadithi iwafae hadhira lengwa. Kwa kubadilisha hadithi na kuzifanya ziwe rahisi kueleweka na kuvutia kwa watoto, usimilisho unawawezesha watoto kujifunza kuhusu mambo mbalimbali kwa njia inayowafaa. Waandsihi wa *Kisa cha Fumo Liyongo* na *Mkasa wa Shujaa Liyongo* wametumia mhusika mkuu Liyongo kama shujaa wa kitendi. Kupitia mhusika Liyongo, mwandishi ameweza kumwonyesha mtoto kuwa, hata Waafrika ni mashujaa na pia wana uerevu. Mhusika mkuu Liyongo katika masimilisho teule ni shujaa wa utendi na mhusika wa kiutamaduni kwa kuwa anasawiri masuala nyeti yanayohusu utamaduni wa jadi wa Waswahili.

Usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto unasaidia watoto kujua kuwa, Liyongo ni mmoja w a mashujaa wa Kiafrika ambaye aliwahi kuishi. Hii ni kwa kuwa, masimukizi yanaeleza kuwa Liyongo ni mmoja wa watu waliowahi kuishi. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa Fumo Liyongo ni shujaa aliyewahi kuishi katika eneo la Upwa wa Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa Jahadhmy (1975), Fumo Liyongo aliishi Kisiwani Pate kati ya karne ya kumi na saba na kumi na nane. Wahakiki akiwemo Mtundura (2001) wanakubaliana kuwa, Liyongo ni mtu aliyeishi katika kipindi fulani cha kihistoria na alikuwa mshairi maarufu na pia shujaa wa vita aliyesifika sana.

Katika *KcFL* na *MwSHL*, simulizi linamrejesha msomaji katika enzi za jadi za Pwani ya Afrika Mashariki, ambapo Fumo Liyongo aliishi kama shujaa na mpiganaji wa haki. Historia ya Fumo Liyongo kama mzalendo anayepinga dhuluma na kupigania haki za watu wake imewasilishwa kwa namna nyepesi na yenye kusisimua, ikilenga kuwapa watoto mfano wa ujasiri, uzalendo na haki. Mambo kama vita vya ukoo, migogoro ya kifamilia na mapambano dhidi ya uonevu yamewekwa katika mtindo wa simulizi la kisasa la watoto.

Katika *WwMK*, historia ya maisha ya mwanamke msomi na mshairi katika karne ya 19 imewasilishwa kwa namna inayomfaa msomaji wa umri mdogo. Badala ya msisitizo wa ushauri wa ndoa pekee, kazi hii imewasilisha maisha ya Mwana Kupona kama mfano wa mwanamke mwenye hekima, anayejua thamani ya elimu, dini na maadili mema. Historia hii inawasilishwa kupitia sura mbalimbali za maisha yake, ambazo zimepangwa kwa njia ya hadithi rahisi, yenye mazungumzo na picha za kisaikolojia zinazowiana na uwezo wa watoto wa kuelewa.

Kwa kutumia alama za kisasa na kubadilisha vipengle katika masimulizi ili kufanana na dhana zinazolenga watoto, waandishi wa masimilisho teule wamewasilisha mawazo kwa hadhira ya watoto kuwa, utamaduni wa kale una nafasi katika utamaduni wa sasa. Kwa kurejelea fasihi ya watoto, tunagundua umuhimu wake katika ukuaji wa mtoto. Hii ni kwa kuwa, fasihi ya watoto haisisitizi tu matumizi ya lugha

bali pia inaunda mazingira ya kiutamaduni ambapo watoto wanaweza kujifunza. Hapa tuanpata kwamba, usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto unaibua umakinifu katika kuandaa watoto wa kizazi kijacho kitamaduni na kihistoria. Kupitia usimilisho, baadhi ya vipengele va mila na desturi za jamii ambazo huleta ugeni au ugumu wa kueleweka kwa hadhira lengwa zimebadilishwa. Katika kazi teule, utafiti huu umebaini kuwa, historia haijawasilishwa kama orodha ya matukio, bali kama sehemu ya maisha ya wahusika. Matukio ya kihistoria huwasilishwa kupitia hadithi za kusisimua, mazungumzo ya wahusika, nyimbo, na visa vya kusisimua vinavyofundisha. Mtindo huu huwahusisha watoto moja kwa moja na kuwafanya washiriki katika historia hiyo kwa njia ya kihisia na kiakili.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Tenzi za kale zimebeba historia, maadili na tamaduni za jamii. Kwa kusimilishwa kuwa fasihi ya watoto kunahakikisha kuwa watoto wanajifunza kuhusu mizizi yao ya kitamaduni na historia, hivyo, kuwajenga kuwa na fahari na kujitambua. Kwa jumla, usimilisho wa tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto ni njia muhimu ya kuhakikisha kuwa watoto wanapata elimu ya kina kuhusu historia na utamaduni wa jamii. Tenzi za kale zimebeba maaadili na mafunzo muhimu. Kusimilisha tenzi za kale kuwa fasihi ya watoto husaidia kupitisha maadili hayo kwa kizazi kipya kwa njia ya kuvutia na inayowafaa watoto. Imebainika kuwa, tenzi za kale zimesimilishwa kuwa hadithi mpya ambazo zinawakilisha utamaduni na historia ya Waswahili kwa watoto. Kubadilisha maandishi ya zamani kuwa fasihi watoto ni njia nzuri ya kuwawezesha watoto kuelewa mambo ambayo hawayaweza kupatana nayo katika maisha yao ya kila siku. Hili limeweza kudhihirika katika vitabu vya *KcFL*, *WwMK* na *MwSHL* kwa kuwa waandishi wa vitabu hivi wameweza kutoa hadithi za zamani kwa kizazi kipya kwa njia ambayo kazi za kiepiki zinaweza kuwakilisha dhana za kisasa katika jamii. Kupitia ubunifu, utamaduni wa kale umebadilishwa ili ufanane na ulimwengu wa watoto kwa njia ambayo watoto wanaweza kujihusisha na utamaduni huo. Kwa kubadilisha tenzi za kale kwa mafanikio, waandishi wamechukua kazi za kale na kuziwasilisha kwa hadhira ya watoto.

**Mapendekezo:** Makala hii inapendekeza watafiti wa baadaye wachunguze kazi nyingine za usimilisho wa tenzi za kale kutoka tamaduni tofauti za Kiafrika.

## MAREJELEO


Baker, M. (2001). *Routledge encyclopedia of translation studies*. Routledge.

Balodis, J. M. (2012). *The practise of adaptation: Turning fact and fiction into theatre* [Doctoral dissertation, Queensland University of Technology]. Queensland University of Technology ePrints. https://eprints.qut.edu.au/60917/1/Janis_Balodis_Thesis.pdf

Bluestone, G. (1957). *Novels into film*. University of California Press.

Dean, J. (2009). Adaptating history and literature into movies. *American Studies Journal, 53*(1).

Hutcheon, L. (2013). *A theory of adaptation*. Routledge.

Jahadhmy, A. (1975). *Kusanyiko la mashairi*. East African Educational Publishers.

Jan, I. (1969). *Children's literature*. Trinity Press.

King'ei, K. (2008). *Wasifu wa Mwana Kupona*. Sasa Sema Publishers.

Lhermitte, C. (2005). A Jakobsonian approach to film adaptation of Hugo's *Les Misérables*. *Nebula: A Journal of Multidisciplinary Scholarship*, 2(1), 97–107. http://www.nobleworld.biz/nebulaarchive/nebula21.html

Matundura, B. (2018). *Mkasa wa Shujaa Liyongo*. Phoenix Publishers.

Mbaabu, I. (Ed.). (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Kenya Publishing & Book Marketing Co.

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi tatu za kale*. TUKI.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Punzi, M. P. (Ed.). (2007). *Literature intermediality: The transit of literature through the media circuit*. International Academic Publishers.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. TUKI.

Wamitila, K. W. (2007). *Kisa cha Fumo Liyongo: Hadithi za mashairi 8*. Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Vide-Muwa Publishers.